# MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA TAREHE 20 JANUARI, 2022.

## WAJUMBE WALIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Wise C. Mgina | Mwenyekiti wa Halmashauri (W) | Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Sunday Deogratius | Mkurugenzi Mtendaji (W) | Katibu |
| 3. | Mhe. Leodgar X. Mpambalyoto | Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri (W) | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Joseph Kamonga | Mbunge wa Jimbo la Ludewa | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Wilbard Mwinuka | Diwani Kata ya Luana | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Robert C. Njavike | Diwani Kata ya Milo | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Joakim J. Lukuwi | Diwani Kata ya Iwela | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Edward Haule | Diwani Kata ya Ibumi | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Daniel T. Mhagama | Diwani Kata ya Masasi | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Elfrida Kizota | Diwani Kata ya Manda | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Edgar Bosco Mtitu | Diwani Kata ya Lubonde | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Florensia Msemwa | Diwani Viti Maalum – Lugarawa | Mjumbe |

## WATAALAM WALIOHUDHURIA

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Bi. Gladness Mwano | Afisa Utumishi na Utawala (W) |
| 2 | Cpa. Theonest Kibuga | Mweka Hazina (W) |
| 3 | Adv. Mathan Chalamila | Mkuu wa Kitengo Sheria (W) |
| 4 | Bw. Mikael F. Hadu | Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 5 | Bw. Israel Malekela | Mkaguzi wa Ndani (W) |
| 6 | Bw. Thomas Kiowi | Afisa Maendeleo ya Jamii (W) |
| 7 | Bw. Isack Makinda | Afisa Mipango Miji na Vijiji (W) |
| 8 | Bw. Gilbert Ngailo | Afisa Ardhi na Maliasili (W) |
| 9 | Bw. Jasper Mkufya | Afisa Uvuvi |
| 10 | Eng. Arafa I. Albert | Mhandisi Ujenzi |
| 11 | Bw. Adili Kayombo | Kaimu Afisa Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji (W) |
| 12 | Dr. Stanley Mlay | Mganga Mkuu (W) |
| 13 | Bw. Florian P. Mtweve | Mkuu wa Idara ya Udhibiti Ubora (W) |
| 14 | Bw. Castory Kibassa | Afisa Usafi na Mazingira (W) |
| 15 | Bw. Daniel John | Afisa Elimu Msingi (W) |
| 16 | Bi. Clementina A. Kabaka | Kaimu Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W) |
| 17 | Bw. Erasmo Mshindo | Afisa Afya (W) |
| 18 | Bw. Peter Kyamene | Afisa Utumishi na Utawala |
| 19 | Bw. Matayo Tematema | Kaimu Katibu TSC (W) |
| 20 | Bw. Kevin Kusenge | Mkuu wa kitengo cha Manunuzi (W) |
| 21 | Bw. Alex Henjewele | Afisa Usafirishaji |
| 22 | Bw. Simon S. Haule | Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 23 | Bw. Salvius Haule | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W) |
| 24 | Bw. Obothe Msemakweli | Afisa Nyuki |
| 25 | Bw. Cyprian Mhagama | Kaimu Katibu wa Afya |
| 26 | Bw. Nicco Mchilo | Kaimu Afisa Biashara |
| 27 | Bw. Peter Liwongwe | Mhasibu wa Mapato |

## SEKRETARIETI

1. Bw. Stephano Moyo
2. Bi. Hilmara Kalaso



Scanned with CamScanner

## MUHT. NA. 60.01.2021 – 22: KUFUNGUA KIKAO

Baada ya akidi ya Wajumbe wa kikao kutimia, Katibu alitoa taarifa ya uwepo wa Mhandisi wa Ujenzi aliyekuja kuanza kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kama ajira mpya. Aidha, alimkaribisha Mhandisi wa Ujenzi ili ajitambulishe na kuwasalimu wajumbe na wataalam. Baada ya kujitambulisha Mhandisi huyo Katibu alimkaribisha Mheshimiwa Mwenyekiti afungue kikao. Akifungua kikao Mheshimiwa Mwenyekiti aliwasalimu wajumbe na wataalam na baadae alimkaribisha Mhandisi wa Ujenzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa na alifungua kikao saa 4:12 asubuhi.

## MUHT. NA. 61.01. 2021 –2022: KUPOKEA AGENDA

Agenda 20 ziliwasilishwa kwenye kikao. Wajumbe walizipokea agenda hizo ambazo ni:-

1. Kufungua kikao.
2. Kupokea agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 23 Disemba, 2021.
4. Yatokanayo na kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 23 Disemba, 2021.
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi kuanzia mwezi Julai, 2021 hadi mwezi Disemba, 2021.
6. Taarifa ya mapokezi ya fedha kwa mwezi Disemba, 2021.
7. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa robo ya pili ya mwaka 2021/2022 kwa kipindi cha kuanzia Oktoba hadi Disemba, 2021.
8. Taarifa ya kitengo cha Manunuzi robo ya pili ya mwaka 2021/2022 kwa kipindi cha kuanzia Oktoba hadi Disemba, 2021.
9. Taarifa ya kitengo cha Ukaguzi wa Ndani robo ya pili ya mwaka 2021/2022 kwa kipindi cha kuanzia Oktoba hadi Disemba, 2021.
10. Taarifa ya kitengo cha Sheria robo ya pili ya mwaka 2021/2022 kwa kipindi cha kuanzia Oktoba hadi Disemba, 2021.
11. Taarifa ya Idara ya Utumishi na Rasilimali watu robo ya pili ya mwaka 2021/2022 kwa kipindi cha kuanzia Oktoba hadi Disemba, 2021.
12. Taarifa ya kitengo cha TEHAMA robo ya pili ya mwaka 2021/2022 kwa kipindi cha kuanzia Oktoba hadi Disemba, 2021.
13. Taarifa ya ujenzi wa jengo la Utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.
14. Taarifa ya ukaguzi wa ujenzi wa bweni la kulala watoto 80 katika shule ya vipaji Ludewa Mjini.
15. Mapendekezo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vinavyotarajiwa kupata mkopo mwezi Januari, 2022.
16. Ombi la kuhuisha Mpango wa Manunuzi wa Mwaka wa Fedha 2021/2022.
17. Maombi ya kuongeza ukomo wa bajeti ya matumizi ya kawaida kutoka shilingi 1,302,822,488.00 hadi kufikia shilingi 1,505,822,488.00 kwa Mwaka wa fedha 2021/2022.
18. Taarifa ya kuungua kwa msitu wa Madope.
19. Taarifa ya ziara ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kukagua miradi ya Maendeleo.
20. Kufunga kikao.



Scanned with CamScanner

**MUHT. NA. 75.01. 2021 –2022: OMBI LA KUHUISHA MPANGO WA MANUNUZI WA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.**

Katibu aliwasilisha taarifa ya kuhuishwa kwa Mpango wa Manunuzi wa Halmashauri ya Wilaya wa mwaka 2021/2022. Alisema Halmashauri iliandaa mpango wa manunuzi wenye thamani ya shilingi 5,460,949,149.85 ambao unatumika hadi sasa lakini Halmashauri imepokea jumla ya shilingi 1,280,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa shilingi 940,000,000.00, ujenzi wa chumba cha wagonjwa mahututi shilingi 250,000,000.00 na ujenzi wa nyumba ya mganga ya "three in one" shilingi 90,000,000.00. Hivyo Mpango wa manunuzi kwa mwaka 2021/2022 utakuwa na thamani ya shilingi 6,740,949,149.85. Baada ya kusema hayo aliwasilisha.

Wajumbe walipitisha ombi hilo na kuridhia kuhuishwa kwa mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha 2021/2022 ili kuwezesha manunuzi ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa, ujenzi wa chumba cha wagonjwa mahututi na ujenzi wa nyumba ya mganga ya "three in one".

**MUHT. NA. 76.01. 2021 –2022: MAOMBI YA KUONGEZA UKOMO WA BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA KUTOKA SHILINGI 1,302,822,488.00 HADI KUFIKIA SHILINGI 1,505,822,488.00 KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.**

Katibu aliwasilisha maombi ya kuongeza ukomo wa bajeti ya matumizi ya kawaida kutoka shilingi 1,302,822,488.00 hadi kufikia shilingi 1,505,822,488.00 kwa Mwaka wa fedha 2021/2022. Alisema maombi haya yanawasilishwa ili kuongeza ukomo wa bajeti ya mapato halisi ya ndani kutokana na hali nzuri ya makusanyo kwa kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi Disemba 2021 ambapo hadi Disemba, 2021 Halmashauri imefanikiwa kukusanya jumla ya shingi 1,041,091,974.99 kati ya shilingi 1,302,822,488.00 zinazotakiwa kukusanywa. Aliendelea kusema kuwa, hivyo bado kiasi cha shilingi 261,730,513.01 ambacho hakijakusanywa ili kufikia lengo la makusanyo ifikapo Juni, 2022. Alisema fedha zinazoombwa kuongezwa kukusanywa ni katika vyanzo vya ushuru wa mbao, ushuru wa viazi na ushuru wa huduma na zitatumika kununua gari, kuchangia shughuli za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2022 na kujenga vibanda vya biashara katika uwanja wa mpira wa miguu wa Ludewa mjini. Baada ya kusema hayo aliwasilisha.

Wajumbe walijadili kuhusu maombi ya kuongeza ukomo wa bajeti ya matumizi ya kawaida kutoka shilingi 1,302,822,488.00 hadi kufikia shilingi 1,505,822,488.00 kwa Mwaka wa fedha 2021/2022 na kukubaliana kuongeza ukomo huo katika vyanzo vilivyoainishwa na matumizi yaliyokusudiwa.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo.

**MUHT. NA. 77.01. 2021 –2022: TAARIFA YA KUUNGUA KWA MSITU WA MADOPE.**

Katibu aliwasilisha taarifa ya kuungua kwa msitu wa Halmashauri uliopo katika kijiji cha Madope. Alisema miti iliyopandwa kwenye msitu huo ni mipaina na wastani wa eneo la msitu lililoungua ni Ekari 30.5 kati ya Ekari 56.35 ya shamba hilo zilizopandwa miti. Baada ya kusema hayo aliwasilisha.

Mjumbe alihoji akitaka kujua hatua zilizochukuliwa dhidi ya mtu aliyetorosha moto. Alishauri kuwa, zichukuliwe hatua za kisheria dhidi ya mtu huyo kwa kupanda miti kwenye eneo ambalo miti imeungua na kuitunza hadi kufikia umri ambao miti hiyo iliungua.



Scanned with CamScanner

Katibu alisema suala lililotokea kwenye ziara ya ukaguzi wa miradi ni bahati mbaya na Mheshimiwa Mwenyekiti amekuwa akitumia magari ya Halmashauri siku zote lakini hakuwahi kutumia gari la namna hiyo ila ni kutokana na changamoto ya uhaba wa magari. Aliongeza kujibu kuwa gari linaloonekana Halmashauri ni gari la Halmashauri ambalo lilitengewa fedha kwenye bajeti ya mwaka 2020/2021. Aliendelea kusema kuwa, Halmashauri imeagiza magari mengine mawili ambayo ni "Hard top" moja na "pick up" moja kwa thamani ya shilingi milioni 257 na Idara ya Elimu Sekondari itakuwa na "Pick up" moja na Idara ya Afya itakuwa na gari moja kwa ajili ya shughuli za UVIKO 19 hivyo changamoto ya uhaba wa magari itapungua.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo.

**MUHT. NA. 79.01.2021 – 2022: KUFUNGA KIKAO.**

Katibu alimkaribisha Mheshimiwa Mwenyekiti ili afunge kikao. Akifunga kikao Mheshimiwa Mwenyekiti alisema mawazo ya wajumbe, ushauri pamoja na maoni yaliyotolewa yafanyiwe kazi kwa mafanikio makubwa ya Halmashauri. Alifunga kikao saa 8:07 mchana.

**UMETHIBITISHWA NA:**

| | |
|---|---|
| **SAINI** ........(signature)........ | **SAINI** ........(signature)........ |
| **JINA** ....WILBERT MTAILO.... | **JINA** ....WISE CHARLES MGINA.... |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |
| **TAREHE** ....28/02/2022.... | **TAREHE** ....28/02/2022.... |